

## **FASIHI YA WATOTO**

\*\*\*

RIWAYA YA KIHISTORIA YA WATOTO, DAFINA ILIYOTELEKEZWA KATIKA FASIHI YA  
KISWAHILI

L.H. Bakize

Taasisi ya Taaluma za Kiswahili

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

leobakize@yahoo.com

### **Ikisiri**

Riwaya ya kihistoria katika fasihi ya watoto ni utanzu unaopendwa na watoto, wazazi na walimu huko Ulaya na Marekani. Utanzu huo unapendwa hasa darasani kwa sababu umekuwa nyenzo muhimu katika kufundishia watoto masomo mbalimbali kama Fasihi, Historia, Jiografia, Lugha, Uraia, na kadhalika. Pamoja na kupendwa kote huko, riwaya ya kihistoria ya watoto katika fasihi ya Kiswahili ni fani ngeni. Ugeni huu unaifanya riwaya hii kuwa nyuma kiutunzi na kiutafiti. Nchini Tanzania, uwanja huu wa riwaya ya kihistoria ya watoto katika fasihi ya Kiswahili uliwekewa misingi na mikakati mizuri miaka ya 1990 lakini hivi leo umetelekezwa na kwa kiasi kikubwa haufahamiki. Aina hii ya riwaya ni muhimu kwa watoto hasa kwa mustakabali wa taifa endelevu na lenye raia wenye uzalendo wa kweli wanaojitambua. Kuitelekeza riwaya ya kihistoria ya watoto katika fasihi ya Kiswahili kunatufanya tukabiliwe na hatari ya kusahau historia yetu; na hivyo, kukosa mwelekeo ufaao. Makala hii inakusudia kuifafanua dhana ya riwaya ya kihistoria ya watoto katika fasihi ya Kiswahili na umuhimu wake kwa watoto na mustakabali wa jamii ya Waswahili.